## Kwako bibi

# Ewe bibi, kwa nini ongezi mchana kutwa ?

Ingawa mmbea (ongezi, commérage) kati ya wanawake laonekana njema ni kwa kuwa lafanyika tu kati ya wanawake wenyewe. Kwani ukipita mikoani utasubutisha kuwa wanawake wamojawamoja hupitisha wakati wao vibaya wakipiga "lisulu" (domo, ongezi) mchana kutwa. Eti "mama fulani njoo kwanza ni kuibie kasiri. Ungelijua kama mama fulani... hum ! Lakini usimwambie mtu mwengine kale ka "sango". Na huyo mama fulani huhaidia kuchunga siri. Lakini punde kidogo huyo mama hutoa siri hiyo nje.

Zoezi hiyo mbaya yatokana na maisha wanayo. Kwani wamama hao hushindia kula na kulala tu kwa kuwa wana watumishi (wabinti, wanawake, wanaume) kazaa wa kazaa wanaowafanyizia kazi zote nyumbani.

Mara nyingi magomvi na vita kali mikoani vyatokana na maongezi hayo yasiyo na maana.

Mara nyingi magomvi na vita kali mikoani kati ya wanawake vyatokana na maongezi hayo yasiyo na maana.

Uvivu wao ni kinyume cha kukosa kazi za kufanya. Wamama wa leo wanao kazi nyingi za kufanya. Ingawa nyumbani kama vile mahali mengine za kazi. Na wanawake wengi hufanya vitendo vinavyowapunguzia heshima.

Wamama wa mtindo huo wakati waamka, hutwa kifagio mkononi, kusokota kikwembe kifuani na kujielekeza kwa mama jirani na huko huanza kuchapa domo, ongezi moja kwa moja kama kasuku. Na tukichungua vizuri mambo hayo, nyumbani vitu vipo ovyo ovyo, vyatupwa huko na huko nafasi visivyostahili, masahani, vyungu, pao na kazalika hushinda vichafu pia. Mavazi hutupwa katika beseni (bakuli) ama "ngalingali" (linjanja, karai).

Fujo hiyo ya vifaa nyumbani ni alama wazi ya kuwa mama wa nyumba hashuruliki na usafi wala usawa wa vitu nyumbani. Basi wewe bibi kwa nini ongezi mchana kutwa ? Na kwa nini washurulika tu na mambo yanayofanywa kwa majirani ao yote yanayopita mikoani ? Kweli kumbe Uvivu na maongezi ya ovyo ovyo ni ya kupiga marufuku kwa kina mama wote.

Bisimwa L.-B. Tserou.

## Koperative ya akiba na mkopo

# Benki kuu ya Zaïre yatia usawa kati

Tokea sasa kila koperative ya akiba na mkopo yapashwa kwanza kupata ruhusa ya Benki kuu ya Zaïre mbele ya kuanza kazi zake. Wakuu wanaohusika na kazi za feza wapo hivi na shuruli ya kutia usawa katika viungo mbalimbali vya mashirika (koperative) yanayofanya kazi zao tangu miaka 12 bila kufanywa uchunguzi kiserikali..

Kwa hiyo, muda wa miezi sita ulipewa kwa mashirika hayo kulingana na taarifa lililotolewa mnamo tarehe 30 Septemba 1985 na Benki kuu ya Zaïre. Taarifa hilo latoa maelezo kamili yanayoweza kupiga marufuku fujo iliotaka kutia mzozo katika maendeleo ya kiungo hicho cha uchumi wa nchi. Uchunguzi wa taarifa hilo waonya kuwa ni lazima kabisa koperative ya akiba na mkopo iwe na kiungo huru kinalopashwa kuhusika pekee na kupana mkopo, iwe atafazali na kiasi cha zaïre 125.000 cha akiba. Kiasi ambacho chapashwa kumilikwa (être géré) na koperative yeyote, kupata ginsi ya kumiliki mikopo na kuwaazibu watu wote watakaojiruhusu kupokonya (kuiba) feza za makoperative.

Yaonekana wazi kama taarifa hilo linalo shuruli la kupana majawabu kwa matatizo mbalimbali yanayoweza kusonga makoperative makuu (COOCEC) na hayo madogo (COOPEC) ingawa maelezo ya taarifa hilo yatafuatwa kama inavyoombwa.

Jimboni mwa Kivu, koperative kuu la akiba na mkopo (COOCEC) baada ya kukataza mkopo wowote ili kupata mwanga kamili katika umiliki (gestion), lilichukua mpango moja maalum wa kurudishwa haki zake na wanamemba waliopewa mikopo ya feza na ambao hukataa kulipa ao hawajalipa bado. Mwito ulifanyika kwa wanamemba hao lakini mpaka sasa hawajali hata kidogo kulipa feza hizo. Na kwa kuwa viongozi wa shirika hilo kuu hawana ginsi ya kuwashtaki wanyanguyangu hao kwani makoperative madogo mamojamoja hayajulikane kulingana na sheria ya Serikali.

Bisimwa L.-B. Tserou.

## Shairi

# Karibu

Karibu mtoto wee
Malkia wa dunia

Watoka wapi
mama wee

Umegawia mbone
Eti ulikuwa mbali ?

Mwaka ulikaribia
Nawe bado kutoka

Wewe peke ulipenda
Wala matako ya Mungu ?

Yote hayo sijali
Umekuja nikakuona

Uso wako kio
macho yako nyota
mwili wako nyororo

Jina lako ni nani sasa?
Jua ?
Mwezi ?
Mwangaza ?
Nyota ?
Chiba au ?

Tafadhali

jina sijapata
karibu tu
karibu mama
wasalimika !

Tangolek.


JUA

*Gazeti la Kivu*

Mwaka wa 12 n° 288 — Tarehe 16 mpaka 22 Novemba 1985

Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara


Tarehe 17 novemba 1985

# Majeshi ya askari yatimiza miaka 25

Siku ya Mungu tarehe 17 Novemba ndipo siku ya ukumbusho wa miaka 25 tangu hapo Jamhuri ya Zaïre kujipatia majeshi yake ya kiaskari.

Wakati nchi yetu ya Zaïre ilijinyakulia uhuru wake mnamo tarehe 30 Juni 1960, majeshi ya askari wetu yalikuwa bado kama yale ya kikoloni (Force Publique). Na wazungu waliokuwa wakiyaongoza walifanya yao yote wakiyachochea ili yatie fujo nchini.

Itajulishwa kuwa wakati ule, waaskari wachache tu ndio walikuwa wakijua kuandika na kusoma. Hali hiyo iliwasukuma wazungu hao kuamsha chuki ya viongozi na aschuki ya viongozi na askari jeshi na hata pia kati ya askari na wakaaji ndugu zao.

Kutokana na mambo hayo, mnamo tarehe 17 Novemba 1960, Mwananchi Mobutu Sese Seko alipokuwa bado akida mkuu wa askari jeshi aliamua vizuri kuunda majeshi mapya ya askari nchini na kuyaunganisha katika umoja. Na hapo jina la zamani "Force Publique" likatengwa na lile la "Armée nationale congolaise" likachukua nafasi mbele lenzie la "FAZ" (Forces Armées Zaïroises) litawale mpaka sasa.

Tangu hapo, siku kwa siku majeshi ya askari wetu yaendelea kusonga mbele. Wavulana (vijana waume) kama vile wasichana (vijana wake) wajielimisha kabisa katika ujuzi wa mambo ya vita na kazalika. Wajitatanua kabisa kujua ginsi ya kutumia silaha za kisasa, kutembeza magari ya chini, vifaru, mashua na ndege za vita na kushurulika zaidi kwa zaidi kujua kutumia vyombo vilivyomo. Shabaa ya mambo hayo yote ni kutia usalama starehe nchini na raïa kuishi bila uwasiwasi wowote, taifa kuepushwa na hatari yoyote itakayoweza kuisaga.

Kumbukumbu ya kuundwa kwa majeshi ya askari tangu miaka 25 itasherekewa nchini mwetu katika furaha na vigelegele. Na wanamapinduzi wote kuwa na kitumaini kwa askari jeshi wao shujaa na kusharikiana nao kwa kumtolea lisala la pongezi la maisha marefu Prezidenti-muundaji wa Chama cha Mapinduzi MPR, Raïs wa Jamhuri, Mareshali wa Zaïre, Baba wa Taifa na Komanda mkuu wa askari jeshi "FAZ", mwananchi MOBUTU SESE SEKO.

Jimboni mwetu mwa Kivu, askari jeshi wakiongozwa na koloneli Akeye waliendesha michezo mbalimbali mbele ya kusomesha misa na kuzindua kantini ya askari katika kampi Saïo. Siku ya Mungu iliyopita, askari wa Kivu walionya Liwali Mwando shamba kubwa ambamo walilima mhogo, mahalagi, mhindi na vinginepo.

Bisimwa L.-B. Tserou.

# Utangazaji wa enjili utafanyika Kinshasa

Mwisho wa mwezi wa Desemba Kanisa la Kristo katika Zaïre kwa njia ya Chuo cha Kristo ulimwenguni (Ministère du Campus pour Christ International) litasimamia mjini Kinshasa mkutano maalum wa utangazaji wa Enjili (évangélisation).

Watu yapata 3000 kutoka nchi mbalimbali za Afrika watahuzuria kwenyi mkutano ule ambao utaendeshwa na wahubiri mashuhuri wanaojulikana duniani kote. Wahubiri hao ni kama BILL GRAHAM, BILL BRIGHT, KASSOUM KEITA na wengine toka Amerika.

Watakaokusanyika mjini Kinshasa ni wachungaji (pasteurs), mapadri wakuu mbalimbali na wakristo wasiokuwa viongozi wa makanisa. Ni hapo wakristo wa Bara la Afrika, la Amerika, la Australia, Azia na Ulaya watatoa ushuhuda wao kulingana na ginsi Yesu Kristo alibadilisha maisha yao.

Inasemekana kuwa mahubiri hiyo ya Kinshasa yatafuatwa duniani kote kila siku kwa muda wa saa mbili kwa njia ya vyombo vya ajabu vinavyoitwa "satellites". Jambo lile laitwa "EXPLO 83".

Kajangu Mususu.